

SILAHA YENYE NGUVU SANA

2Kor.10:3-5

Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome; tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo;”

[1] Maombi:

Sasa, katika safari hii Ameahidi kutupatia kila kitu ambacho tunakihitaji. “Chochote utakachomwomba Baba yangu kwa Jina langu, hilo nitalifanya. Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” (Marko 11:24). Sasa, ametupa sisi silaha yenye nguvu sana ambayo imewahi kuwako katika dunia yote, na hiyo ni maombi. Maombi ndiyo yanayobadilisha mambo. Mkristo hatambui nguvu aliyonayo wakati anapopiga magoti mbele za Mungu mwenye enzi katika Jina la Yesu Kristo. Hatambui hiyo nguvu ilivyo. Kama watu wangetambua tu kile hasa walichopewa, chochote uombacho utapewa kama unaweza kukusanya imani ya kuamini hilo. Kwa maana Neno la Mungu ni kweli.

Kile watu wanachoita kuwa ni kikuu, Mungu anakiita ni upumbavu na kile watu wanachoita upumbavu, Mungu anakiita kikuu. Kwa hiyo tunachopaswa kufanya ni kurudi kwenye utaratibu wa Mungu na kutafuta katika yote, kile Mungu anachotaka tufanye. Na jambo pekee nijualo la kufanya ni kuomba. Maombi ni ufunguo. Hilo ni Jibu. Maombi yanageuza mambo. Maombi ni silaha yenye nguvu kuliko zote ambayo imewekwa katika utawala wa mwanadamu. Hakuna bomu la Atomiki, au bomu la hewa mlipuko (hydrogen) lenye nguvu kama nguvu ya maombi. Maombi yanabadilisha mawazo ya Mungu. Je ulijua hilo? Ilifanya hivyo wakati mmoja.

Nabii alitumwa kwa mfalme katika chumba chake cha ndani, na akaambiwa nenda ukamwambie mfalme, “BWANA ASEMA HIVI, Hataondoka hapo kitandani, atakufa hapo hapo alipo”. Isaya akaenda na kumwambia Hezekia hayo na nawazia wakuu wote pale mlangoni, wakulima nje huko ya lango walipoingia ndani walisema “Ee Nabii wa Mungu, ni nini yatakayompata mfalme wetu?”

BWANA ASEMA HIVI, yeye ataenda kufa” (2Wafalme 20:1-7).

Alienda nje kwa askari, Eee nabii mkuu, Mungu anasema nini kuhusu Mfalme wetu?” BWANA ASEMA HIVI, yeye atakufa”. Na hiyo ilikuwa ni kweli; Bwana alimwambia hivyo. Naye anaenda chini, anaingia katika kibanda chake kidogo mahali fulani nyuma kule porini.

Na Hezekia akageuza uso wake ukutani na kulia sana sana, na kusema, “Bwana Mungu, kumbuka haya nakusihi unifikirie mimi; Nilivyokwenda mbele zako kwa ukamilifu wa moyo. Nahitaji miaka kumi na mitano zaidi kuuweka ufalme wangu katika hali nzuri. Na unajua, Mungu angetaka kumuambia chochote, angemwambia wakati alipokuwa akizungumza naye. Lakini Mungu ana njia za kufanya mambo. Unapaswa uje katika njia ya Mungu na namna ya Mungu ya kufanya mambo. Na ili mradi tunajaribu kuingia katika hilo sisi wenyewe haitatenda kazi (haitafanikiwa) hatuwezi kujilinganisha mmoja kwa mwingine; inabidi tuishi kila mtu kibinafsi mbele za Mungu.

Sasa, mtu mkuu sana katika nchi, kwa hakika alikuwa ni mfalme na mtu mkuu sana mbinguni alikuwa ni Mungu. Pale alikuwapo mtu mkuu sana duniani akizungumza na mtu mkuu sana mbinguni. Mkuu sana mbinguni, na bado nguvu kuu za mbinguni hazikuweza kuzungumza hapa na mfalme. Kwa maana hakukusudiwa kuwa hivyo; yeye alikuwa tu ni mfalme. Na hapo yeye akazungumza na Isaya (ambaye alikuwa ni Nabii wake) na kusema, “Nenda ukamwambie nimesikia maombi yake nami nitamwongezea hiyo miaka kumi na mitano” Sasa unafikiriaje jinsi yule nabii alivyoona kutwezwa kurudi tena. Unafuata nini tena Nabii? Ungelifikirije Isaya akija katika lile kusanyiko?

Na Mungu alimwambia tena, “Nenda urudi nyuma ukamwambie hatakufa”. Kumetokea nini? Maombi. Silaha kubwa sana iliyowahi kuwekwa katika mikono ya mwanadamu.

Naweza kumuona Isaya akitembea kurudi na kusema “Narudia usemi wangu, hatakufa yeye ataishi. HII ASEMA BWANA, yeye ataishi. HII ASEMA BWANA”. Nini kimefanya hivyo? Nini kimebadilisha? Maombi.

Hiyo ndiyo siri. Maombi yanafungua mlango; maombi “Yo yote myaombayo mkisali, mkiwa na imani, mkiamini, mtapokea. Ombeni kwa wingi ili furaha yenu itimilike”

Kwa hiyo ndiyo sababu alisema “Maombi ya imani yatamuokoa mgonjwa” maombi yale ya binafsi. “Maombi yake mwenye haki yafaa sana akiomba kwa bidii” (Yokobo 5:16).

Oh, kama tu ungalijua, kwamba mikononi mwetu Kristo ametupa sisi mamlaka kwa Jina lake kwa kuwa Wakristo, nguvu kuu sana iliyowahi kujulikana duniani: Maombi, yanageuza kila kitu, yaligeuza mawazo ya Mungu, yalifanya hivyo. Somo Efeso 5:18-20; Rumi 15:30-32 na 2Wathesalonike 3:1-2.

[2] Kujikabidhi na Kukiri

Neno la Mungu litamshinda shetani popote pale, sehemu yoyote, wakati wowote. Sasa, Yesu alipokuwa hapa duniani, ninaamini Yeye alikuwa, vema. Alikuwa ni

Immanueli. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake mwenyewe (2Kor. 5:19). Kwa hiyo tabia zote kuu za Baba zilikuwa ndani ya mwana Kristo Yesu alipokuwa hapa duniani. Vyote alivyokuwa navyo Baba ni vyake. Na vipawa vyote vizuri alivyokuwa navyo Mungu, na vyote vilivyowahi kuwa, vilikuwa ndani ya Kristo. Lakini alipokutana na shetani. Hakutumia chochote cha hivyo vipawa. Yeye, anapaswa kuwa mfano wako, Aliileta mahali ambapo Mkristo aliye mdhaifu sana alisema sasa, yeye alikuwa na nguvu pale za kuweza kumkemea shetani na kumfukuza aende zake. Lakini alichofanya, hakutumia kamwe yoyote ya nguvu zake.

Mara watu wanaona aibu. Baada ya kumkubali Bwana Yesu kama mwokozi wao, wanaenda nje kule na wanaona aibu kumkiri Yeye hupaswi kamwe kumuonea aibu Yeye. Unapaswa kuhusika kikamili haijalishi kunatokea nini, unapaswa kuwa mstari wa mbele kusimamia ushuhuda wako.

Kwa maana Mungu anaweza tu kukuokoa kadiri unavyoshuhudia. Anaweza tu akakuponya kadiri unavyoshuhudia. Yeye ameketi mkono wa kuume wa Baba usiku leo kufanya upatanisho kutokana na maungamo yako. Siyo vile unavyolia kwa sauti, unavyopiga madhabahu kwa nguvu, matendo mengi mazuri unayofanya; ni imani yako inayokuokoa wewe.

Na kama utaikiri kwa midomo yako na kinatoka moyoni mwako, anaenda kufanya kazi kama kuhani mkuu aliyeketi mkono wa kuume wa Baba kufanya upatanisho juu ya maungamo yako. Waebrania 3:1. Hawezi akakufanyia jambo moja lolote mpaka kwanza umeliadini hilo na kulikubali na kulikiri kwamba liko hivyo.

Na watu leo, wataenda nje na kusema, “vema, nilijisikia vizuri usiku wa jana. Lakini leo najisikia vibaya kiasi kwamba siwezi kustahimili hilo”. Hiyo ni sawa kabisa na unapopoteza kukiri kwako na kuanguka chini pale. Haijalishi wewe ni nani, umtakatifu kiasi gani, umtaua kiasi gani, wewe ni mhudumu, kiongozi wa dini, au shemasi, au chochote ulicho, au umekuwa mkristo kwa miaka hamsini, kama unaondoka hapa kesho na kupoteza imani kwamba wewe ni mkristo na ukaanza kuwaambia watu kuwa wewe siyo mkristo tena, umerudi nyuma, umepotea.

Ni kwa kukiri kwako unakuwa umeokolewa. Hivyo ni silaha yenye nguvu kuu sana Mungu aliyoiweka katika mkono wa mtu, ni kujikabidhi (Zaburi 37:5 na Zaburi 55:22) na kukiri (Waebrania 3:1-2) na (Waebrani 4:14 -16). Itatenda hivyo kila mara, kama utaiadini – hiyo na kuikubali kwa msingi huo, na kuiadini na kuishikilia hiyo. Endelea kukiri hilo. Unapokiri hilo (Matayo 10:32).

Unajua kile watu wengi wanachoangalia ni dalili wanazunguka wakisema, “ vema sasa, sijisikii vizuri chochote” Hilo halihusiani hata mara moja na hilo. Ni kile unachoamini, sio kile unachojisikia.

[3] Ubatizo wa Roho Mtakatifu ndani ya mioyo yetu:

Wanaume na wanawake, tunachohitaji leo siyo majina yetu katika kitabu cha kanisa, ambacho ni jambo zuri tu, lakini tunahitaji kuchukua ile silaha kuu ya Roho Mtakatifu ndani ya mioyo yetu, ambayo inabadilisha utu wetu wa ndani na kutufanya viumbe vipya ndani ya Kristo Yesu, na kuweka njia ya kupita katika ulimwengu huu wa dhambi kwa haki na nguvu ya kufufuka kwa Yesu Kristo.

Hicho ndicho tunachohitaji. Hicho ndicho kanisa linachohitaji, siyo kuinua nyuso au kundi la wanachama wanya, lakini kufufusha/kuamsha kile tulicho nacho, na kujazwa na Roho Mtakatifu, na kuandaliwa kupambana na adui, kuombea wagonjwa, kuponya wagonjwa, na kutoa pepo. Mmepewa bure; toeni bure. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio (Marko 16:17-18).

Kristo ameweka kwenye mikono ya watu silaha yenye nguvu sana iliyowahi kuwekwa kwa wanadamu, ilikuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu; moyo mpya, roho mpya. “Nami nitaweka Roho yangu pale” (Ezekieli 36:26 – 27). Na hapo sasa pambana kwa kutumia ulicho nacho mpaka kifo kitakapokuweka huru.

Yeye alimtumia tena siku ya Pentecoste kwa uzao ulioanguka wa Adamu, ubatizo wa Roho Mtakatifu, alisema: “Chukua hii na fanya kwa uwezo wako wote kupambana uondoe ujinga, na imani za kishirikina, dhambi na magonjwa”. Wanaume wanaodai kubusu viwango vya kikombe cha baraka za Mungu, tutawezaje kutulia katika wakati kama huu wakati Mungu ametupa silaha zenye nguvu sana ambazo zimewahi kuwekwa mkononi mwa mwanadamu kupambana na dhambi, na magonjwa, na ujinga na ushirikina na mambo kama hayo. Ni anga halisi lililojaa ubatizo halisi wa Roho Mtakatifu. Mungu anataka mashujaa. Je wewe utakuwa mmoja wao?

[4] Upendo wa Mungu:

Bado hatujafikia kiini chenyewe. Ni Yesu Kristo Upendo wa Mungu, ambao Mungu anataka sisi tuone. Jambo la kuhunzisha. Upendo ndio mkuu, silaha yenye nguvu sana ambayo dunia hii imewahi kuona au imewahi kufahamu. Upendo wa Mungu uliomiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu. Upendo wa Mungu kwetu (Rumi 5:5).

Ninao msemu: Fanya lililosahihi; ni wajibu wako kwa Mungu. Fikiri yaliyo sahihi; huo ni wajibu wako kwako mwenyewe. Na utakuwa uko sahihi”. Na kama utajizoeza kufanya jambo sahihi (unaona), itakuwa likikuzunguka kama mche wa mzabibu; litakuwa linakuvuta ndani yake. Na kama huwezi ukampenda adui yako kama vile uwapendavyo wale wakupendao, kuna kitu sio sahihi mahali fulani unaona?

Sasa, hebu fikiriri: “Ni wajibu wangu kumpenda adui yangu” Unapaswa umpende kweli kweli. Lakini ngoja nikuambie siri ndogo. Nguvu iliyo kuu sana kuliko zote katika dunia siyo kunena kwa lugha, au kutafsiri lugha, au kuheshimiwa na Mungu na kuwa mhuduma, au kuwa mwinjilisti, au kuwa Nabii; nguvu iliyo kuu sana kuliko zote nilizoziona maishani mwangu, ni upendo. Upendo wa Fileo, ni neno la kigiriki

linalotokana na urafiki, kama vile mke wako. Kuna tofauti itamfanya mama kwa ajili ya mtoto, akimbie kupitia moto unaowaka. Maisha yake hayamaanishi kitu. Huo ni fileo. Agape utafanya nini? (unaona?) upendo wa kimungu.

Lazima tuwe na upendo, kupendana kimungu mmoja kwa mwingine. Hapo sasa huoni makosa ya ndugu yako (1Yohana 2:10; Mithali 17:9). Kama alifanya makosa, kamwe, unaangalia juu ya hayo, na kwa vyovyote unampenda. Unaona? Hiyo ndiyo hasa. Wapende wale wakupendao wewe je na mwenye dhambi si anafanya hivyo? Lakini kuwapenda wale wasiokupenda. Hicho ndicho kinacho onyesha Roho wa Mungu yako ndani yuko, kwa sababu alikupenda wewe ulipokuwa adui yake. Na Yeye alikupenda. Na hiyo Roho iko ndani yako, itakufanya uwapende maadui zako, kama ufanyavyo marafiki zako Matayo 5:43-48).

Roho ovu hazitolewi kwa ukatili wa maisha tofauti. Nguvu kuu sana kuliko zote iliyopo duniani ni upendo (1Kor.13:1-13, 2Kor.5:14).

Niweke karibu na pazia, chini ya damu ya Bwana Yesu, Chukueni karama zenu; ambaazo mnazo katika maandiko. Shetani anaweza akaigiza kila moja ya hizo; lakini hawezi akaigiza upendo, kwa sababu upendo ni kitu halisi. Shetani hawezi kupenda, hilo ni jambo moja hawezi kufanya. Na mkifikia mahali ambapo mnapendana mmoja kwa mwingine, na dunia yote imekufa Na kama unapenda Mungu..... (Yohana 13:34 – 35).

Nukuu za Kiingereza:

Malaika wangu ataenda mbele zako (53-0213), aya 7-9/Matarajio (61-0207), Aya 9 – 10/kufufuka kwa binti wa Yairo (54-0302), Aya 49/ kumuamini Mungu (52-0224), Aya 107/kwa Neno lako, Bwana” (54-1207) Aya 46 – 48/ Ugizaji wa ukristo (57 – 0127A, Lima), Aya 66/msikilizeni Yeye 58-0301E – Chottanooga), Aya E – 63/Msikieni Yeye (57-0322, Oakland) Aya 51/ Tangu wakati ule (61-0415B, Bloomington), Aya 25 – 27/ kwa nini watu wanayumbishwa huku na huku (56-0101), Aya 86 – 89, uk. 28 – 30.

Jiwe la Kiroho la kujengea na III kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69, D-75328 Schomberg, Germany, Simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk. 724).

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,
Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: Chaelika@livel.com
Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*